Muhtasari Mfupi wa

Jimbo la New York

Sheria ya Leseni ya Dereva ya Kuhitimu (GDL)



Mwongozo wa Mzazi

Jimbo la New York

kaunti zote isipokuwa

Jiji la New York na Long Island

KUMBUKA: Mwongozo huu unaandalia muhtasari mfupi wa GDL. Kwa habari ya kina, wazazi wanapaswa kutembelea tovuti ya DMV kwenye DMV.ny.gov.

Kabla ya kijana wako ataanza kuendesha gari,
kuna mambo machache ninyi wawili mnahitaji kujua.

Habari mbaya: Kwa sababu ya kukosa uzoefu, vijana wana uwezekano mkubwa zaidi wa kupata ajali.

Madereva vijana wanahusishwa na ajali zaidi kuliko vikundi vingine vya umri. Ajali zinazohusisha vijana pia zinaweza kuwa mbaya zaidi. Mwaka wa kwanza wa kuendesha gari bila usimamizi ni hatari zaidi kwa sababu ya ukosefu wa uzoefu.

Habari njema: Sheria za Leseni ya Dereva ya Kuhitimu Zinaokoa Uhai

Ajali zinaweza kuzuiwa. Sheria ya Jimbo la New York (NYS) ya Leseni ya Dereva ya Kuhitimu (GDL) imeundwa kuzuia ajali za vijana kwa kuwasaidia vijana kujenga ustadi wao polepole na kwa usalama na kupata uzoefu wa kuendesha gari. Unahitaji udhibitisho?

Sheria ya NYS GDL imesababisha kupunguza ajali kwa 80% kwa madereva ya miaka 16 na 17. Kuna sababu kwa kila kizuizi katika sheria (mpaka wa idadi ya abiria, saa za kuendesha, na kadhalika.)

Utafiti unaonyesha kwamba mbinu hizi zinafanya kazi.

Unaweza kufanya nini ili dereva kijana wako awe salama?

Kijana yako anapoendesha gari, wewe ni zaidi ya abiria. Wewe ndiye mshawishi #1 kwa dereva wako kijana. Tumia mwongozo huu kufahamu sheria ili unaweza kumsaidia dereva wako kijana kusafiri kupitia barabara na pia kushughulikia mchakato wa kupata leseni isiyo na vizuizi!



Mwongozo huu unafafanua vizuizi vya GDL kwa kibali cha dereva kijana na wenye leseni ya kijana wanaoendesha katika jimbo la New York (kaunti zote bila jiji la New York na Long Island).

Vizuizi vinatumika katika eneo ambapo kijana yako anaendesha, si ambapo mnaishi.

Hatua za leseni

Kuna hatua tatu za leseni kwa madereva vijana:

1 Kibali cha Kijana/ Kibali cha Kijana cha Pikipiki

- Umri wa chini ni 16.
- Anahitaji kupita mtihani wa maandishi.
- Lazima awe na usimamizi wa mzazi anapoendesha.
- Ona ukurasa wa 3 kwa habari zaidi.

2 Leseni ya Kijana/ Leseni ya Kijana ya Pikipiki (vizuizi)

- Inaruhusu kuendesha bila usimamizi na vizuizi vya saa na abiria.
- Ona ukurasa wa 5 kwa habari zaidi.

3 Leseni ya Dereva Asiye na Vizuizi/ ya Pikipiki

- Umri wa chini ni 18, au umri wa 17 na elimu ya dereva.
- Hiyo ndiyo leseni bila vizuizi (si chini ya vizuizi vya GDL).
- Ona ukurasa wa 9 kwa habari zaidi.

Kupita hatua zote tatu za leseni kunampatia kijana yako wakati na uzoefu anaohitaji ili kuwa dereva salama zaidi.

Kumbuka: Kama kila kitu kingine, unamjua mtoto wako vizuri zaidi. Vizuizi vinavyofafanuliwa katika mwongozo huu ni sheria za chini za usalama ambazo kijana yako anapaswa kufuata. Unaweza kuchagua kumzuia zaidi ikiwa unahisi kwamba mtoto wako hayuko tayari kwa madaraka ya ziada ya kuendesha.

HATUA 1: KIBALI CHA KIJANA

Hiki ni kipindi cha kujifunza. Inawaruhusu madereva vijana kujifunza misingi ya kuendesha gari kupitia kuendesha kwa vizuizi.

Kujaza ombi la kibali cha kijana, mtoto wako anapaswa:

- Awe na umri wa 16 au zaidi.
- Awe na udhibitisho wa utambulisho (kwa mfano, pasipoti, kadi ya usalama wa kijamii) na ailete kwa mtihani.
- Ajifunze Kitabu cha Dereva cha Jimbo la New York (nakala zilizochapishwa za Kitabu zinapatikana kwenye ofisi za DMV za eneo lako na kitabu cha mtandaoni kinapatikana kwenye http://dmv.ny.gov/driver-license/drivers-manual-practice-tests).
- Jaza ombi (fomu ya DMV MV-44).
- Pita mtihani wa maandishi na mtihani wa macho.

Kwa habari zaidi kuhusu kupata kibali cha kijana, mtihani, fomu, na ada, tembelea tovuti ya NYS DMV kwenye:

http://dmv.ny.gov/driver-license/get-learner-permit

Saidia kijana yako afanikiwe!

Kabla ya kijana wako ataendesha, keti pamoja naye na unda makabiliano ya kuendesha gari kwa usalama, kuweka sheria, na matokeo kwa kuzivunja. Kwa makubaliano ya mfano, tembelea:

www.safeny.ny.gov/SRO-Toolkit/contract.html

Sasa mazoezi ya kuendesha yanaanza!



Jambo moja muhimu zaidi la kuwa dereva salama ni kufanya mazoezi. Kabla ya kijana yako anaweza kufanya mtihani wa barabara, anapaswa kumaliza **angalau** saa 50 za uendeshaji unaosimamiwa ulioidhinishwa na mzazi, na 15 za saa hizo zinahitajika baada ya jua kutua. Tumia Rekodi ya Mazoezi ya Kuendesha kufuatilia namba ya saa ambazo wewe na kijana yako mmeendesha pamoja. Pia unaweza kutaka kuandika chini ustadi uliotumia, uliozoea, na mpya wa kufanyia kazi zaidi. Rekodi inapatikana kwenye ukurasa wa 25 wa Mwongozo wa Rasilimali wa Dereva Kijana wa NYS kwenye:

http://www.nxtbook.com/nxtbooks/nysdmv/teenresourceguide/#/30



Vizuizi vya Kibali cha Kijana
Kaskazini mwa New York

Shughuli Inayoruhusiwa = ✓ Shughuli Ambayo Hairuhusiwi = X

	Mchana Saa11 asubuhi-saa3 usiku	Usiku Saa3 usiku-saa11 asubuhi
Wenye kibali cha kijana wanaweza kuendesha gari chini ya usimamizi tu	✓ Anapaswa kuwa chini ya usimamizi wa mwenye leseni ya NYS wa miaka 21 au zaidi.	✓ **Anapaswa kuwa chini ya usimamizi wa mwenye leseni ya NYS wa miaka 21 au zaidi ambaye ni mzazi, mlezi, mwalimu wa elimu ya dereva/ mwalimu wa shule ya dereva, au mtu aliyeteuliwa *in loco parentis*[1].**

- Hakuna abiria wa mbele isipokuwa dereva anayesimamia.
- **Pamoja na mzazi/mlezi kama dereva anayesimamia:** hakuna vizuizi vya namba ya abiria wanaoketi nyuma. **Ikiwa dereva anayesimamia si mzazi/mlezi (mchana peke yake):** abiria mmoja tu chini ya 21 anaruhusiwa, isipokuwa abiria ni familia ya karibu.
- Kila abiria anapaswa kutumia mkanda wa usalama na kila abiria mtoto anapaswa kutumia kiti cha mtoto sahihi. Kwa habari zaidi kuhusu Sheria ya Kizuizi cha Abiria ya NYS, tembelea www.safeny.ny.gov/sesa-ndx.htm.
- Kwa wenye kibali kuendesha katika jiji la New York, gari inapaswa kuwa na udhibiti mbili (breki mbili). Ona mwongozo wa NYC GDL kwa vizuizi vya ziada. Kuendesha hairuhusiwi kwenye barabara kuu za Cross County, Hutchinson River, Saw Mill River, au Taconic State, kwenye barabara yoyote ndani ya mbuga wa NYC, au kwenye daraja au handaki lolote chini ya mamlaka ya Tri-borough Bridge and Tunnel Authority.
- Kibali cha kijana kwa leseni ya pikipiki: dereva anayesimamia anapaswa kuwa na leseni ya dereva halali ya kuendesha pikipiki kijana yako anayoendesha, na anapaswa kufanya usimamizi wa jumla na udhibiti kwa kubaki ndani ya robo moja ya maili. Hakuna abiria anaruhusiwa isipokuwa yule abiria ana leseni ya pikipiki halali isiyo na vizuizi.

Adhabu: faini $75-$300 Jela: mpaka siku 15

in loco parentis[1] = Mtu ambaye mara kwa mara/kupanuliwa, amekubali tabia ya mzazi na anatimiza majukumu ya mzazi kwa sababu ya kifo, ulemavu, au kutokuwepo kwa mzazi asili.

Kuanzisha Hatua 2 (leseni ya kijana) kijana yako anapaswa:

- Kuwa na kibali chao cha kijana kwa miezi sita au zaidi.
- Kufanya darasa la kabla ya leseni au darasa la elimu ya dereva (pia inaitwa "darasa la saa 5."
- Maliza saa 50 za uendeshaji unaosimamiwa ulioidhinishwa na mzazi, na saa 15 za saa zile zinaitaji kuwa baada ya jua kutua, kabla ya kufanya mtihani wa barabara.

  (Rekodi ya mazoezi inapatikana kwenye ukurasa wa 5 wa Mwongozo wa Rasilimali wa Dereva Kijana wa NYS kwenye http://www.nxtbook.com/nxtbooks/nysdmv/teenresourceguide/#/30)
- Jaza fomu ya DMV MV-262 Udhibitisho wa Kuendesha Gari ya Kusimamiwa. http://dmv.ny.gov/forms/mv262.pdf
- Panga mtihani wa barabara na kuifanya.

HATUA 2: LESENI YA KIJANA

Hiki ni kipindi cha kuzoea. Inamruhusu dereva kijana kufanya mazoezi na kuboresha masomo amejifunza wakati wa hatua ya kibali cha kijana. Mapendeleo ya ziada yanaanza katika hatua hii.

Vizuizi kwa wenye leseni ya kijana vinavyofafanuliwa katika mwongozo huu ni sheria za chini za usalama ambazo kijana yako anapaswa kufuata. Unaweza kuchagua kumzuia zaidi ikiwa unahisi kijana yako hayuko tayari kuendesha gari.



Vizuizi vya Leseni
Kaskazini mwa New York

Shughuli Inayoruhusiwa = ✓ Shughuli Ambayo Hairuhusiwi = X

Wenye leseni ya kijana wanaweza kuendesha bila usimamizi:	**Mchana Saa11 asubuhi-saa3 usiku**	**Usiku Saa3 usiku-saa11 asubuhi, moja kwa moja kuenda na kutoka nyumbani:**
Madarasa ya Shule[2]	✓	✓
Kazi	✓	✓
Shughuli nyingine zote kutia ndani shughuli za shule baada ya masomo, michezo, na matukio ya kijamii	✓	X

Kwa shughuli zilizoidhinishwa, kijana yako anapaswa kuwa na hati zilizosainiwa na mwalimu au mwajiri.

Kijana yako **haruhusiwi** kuendesha wakati wa kazi (kusafirisha, kadhalika).

Kwa shughuli zote za usiku, kijana yako anaweza kuendesha na dereva anayesimamia[3].

- **Bila dereva anayesimamia[3]:** abiria mmoja tu chini ya miaka 21 anaruhusiwa, isipokuwa abiria ni familia ya karibu. **Pamoja na dereva anayesimamia[3]**: hakuna vizuizi kwa namba ya abiria.
- Kila abiria anapaswa kufunga vizuri mkanda wa usalama au kiti cha usalama wa mtoto.
- Leseni ya kijana ya pikipiki: dereva anayesimamia anahitaji kufanya usimamizi wa jumla tu na udhibiti juu ya mwanafunzi anapoendesha pikipiki. Hakuna abiria anaruhusiwa isipokuwa yule abiria ana leseni halali ya pikipiki isiyo na vizuizi.
- Kunendesha jijini NYC, kwa sababu yoyote, kumekatazwa ukiwa na leseni ya kijana. Kwa kuongezea, hakuna kuendesha gari barabarani yoyote katika mbuga wa NYC, kwenye daraja au handaki lolote chini ya mamlaka ya Tri-borough Bridge and Tunnel Authority, au barabara kuu za Cross County, Hutchinson River, Saw Mill River, au Taconic State.

Adhabu: faini $75-$300 Jela: mpaka siku 15

Darasa la Shule[2] = Ufundishaji, elimu au mafunzo yameyoidhinishwa au kukubaliwa na shirika la serikali au idara, au mafunzo yanayoongozwa na Majeshi ya Marekani. Maneno "darasa la shule" hayatia ndani shughuli za baada ya masomo, michezo au matukio ya kijamii ambayo hakuna mikopo ya kielimu yanayotolewa.

Dereva Anayesimamia[3] = Mwenye leseni ya NYS wa miaka 21+, ambaye ni mzazi, mlezi, mwalimu wa elimu ya dereva/mfundishaji wa shule ya dereva, au mtu aliyeteuliwa *in loco parentis*.

Kusimamishwa & Kuondolewa

Kutumia kifaa elektroniki anapoendesha ni dhidi ya sheria kwa madereva yote.

Adhabu:

Hukumu ya kwanza ya matumizi ya simu ya mkononi au uhalifu wa kuandika inasababisha kusimamishwa kibali cha kijana kwa siku 120 na pointi 5.

Hukumu ya pili kati ya miezi sita ya kurudishwa kibali inasababisha kuondolewa kibali angalau mwaka moja kwa kibali na pointi 5.

Chini ya "Sheria ya Uvumilivu Sifuri" ya NYS, dereva chini ya 21 hawezi kuendesha kisheria akiwa na kiwango cha pombe katika damu cha .02 au zaidi (kiwango kinachoweza kutokea kutokana na kutumia dawa ya kinywa au ya kukohoa.)

Adhabu:

Kusimamishwa leseni kwa miezi 6, adhabu ya raia ya $125, na ada ya kukomesha kusimamishwa ya $100.

Kila kosa la ziada litasababisha kuondolewa kibali cha kijana kwa angalau mwaka moja au mpaka umri wa miaka 21 (yoyote ambayo ni zaidi), pamoja na adhabu ya raia ya $125, na ada ya maombi ya kibali upya ya $100.



Nini kinatokea ikiwa ana zaidi ya moja ya uhalifu zifuatazo?

Kibali cha kijana au leseni ya kijana yako itasimamishwa kwa siku 60 ikiwa amehukumiwa kwa uhalifu mbili unaofanywa wakati alikuwa na kibali cha kijana au leseni.

Pia leseni yao itasimamishwa kwa siku 60 ikiwa amehukumiwa kwa moja ya "uhalifu mkubwa wa barabarani" (kwa kawaida ina pointi tatu au zaidi), kwa mfano kuendesha gari kwa kasi sana au kutuma ujumbe fupi anapoendesha. Baada ya kusimamishwa kumalizika, ikiwa dereva kijana yako anahukumiwa ndani ya miezi 6 kwa uhalifu moja mkubwa wa barabarani au uhalifu mbili mwingine, kibali chao cha kijana kitaondolewa kwa siku 60.

Ikiwa leseni imesimamishwa, kijana yako anaweza kuendesha tena baada ya kipindi cha kusimamishwa kimekwisha. Ikiwa leseni imeondolewa, basi imepotea kabisa, na kijana yako atapaswa kuanza tena na kujaza ombi la leseni baada ya siku 60.

Chunguza jinsi kijana yako anavyoendesha gari!

Jiandikishe katika Pogramu ya TEENS na NYS DMV - utapokea taarifa wakati matukio maalum (tiketi, uhalifu wa barabarani, kusimamishwa leseni ya dereva, na ajali fulani) yanaongezwa kwa rekodi ya kuendesha ya kijana yako.

http://dmv.ny.gov/dmv-records/monitor-my-teen-driver-teens

Unadhibiti funguo.

Kama mzazi au mlezi aliyekubali utoaji wa kibali cha kijana au leseni kwa kijana yako, una haki ya kufuta kibali au leseni ya kijana yako ikiwa unahisi hapaswi kuruhusiwa kuendesha. Jaza fomu ya DMV MV-1W (Kuondoa Kibali) na wasilisha kwa DMV.

http://dmv.ny.gov/forms/mv1w.pdf



HATUA 3: LESENI ISIYO NA VIZUIZI

Leseni kamili, bila vizuizi itatumwa kwa barua kwa yeyote mwenye leseni ya kijana baada ya siku yake ya kuzaliwa ya miaka 18. Leseni isiyo na vizuizi ni liseni ile ile ambayo watu wazima wanayo na inamruhusu kijana yako kuendesha popote katika NYS bila vizuizi vya saa au abiria.

Vijana ambao wamechukua darasa la elimu ya dereva:

Kijana yako anaweza kujaza ombi kwa leseni yake kamili kwa umri wa miaka 17 ikiwa alipokea Cheti cha Mwanafunzi cha Kumaliza (DMV fomu MV-285) kutoka darasa la elimu ya dereva lililokubaliwa. Mara tu dereva yako mwenye miaka 17 amepita mtihani wake wa barabara na kuwasilisha MV-285 kwa DMV anapewa leseni. Ikiwa kijana yako hawasilishi fomu yake ya MV-285, bado atakuwa mwenye leseni ya kijana na anapaswa kuendelea kufuata vizuizi vya GDL.

Kuendesha gari kwa usalama kunahitaji mazoezi

Kupewa leseni isiyo na vizuizi si mwisho wa kujifunza kuendesha. Inachukua miaka, kabla ya mtu ni mwenye stadi wa kuendesha gari. Vijana wanaweza kujua watu shuleni au kutoka shule nyingine ambao wamekufa au wamejehuriwa vibaya katika ajali. Bado vijana wana hatari kubwa kuliko idadi ya watu kwa ujumla. Wahimize kuendelea kujifunza na kuzoea tabia salama ya kuendesha.





MAMBO MAKUU

KIBALI CHA KIJANA

- Mazoezi, mazoezi, mazoezi.
- Anaweza kuendesha tu pamoja na dereva anayesimamia.
- Anapaswa kungoja angalau miezi sita kabla ya kfanya mtihani wa barabara.
- Ikiwa anaendesha gari katika NYC, anapaswa kuwa na gari lenye breki mbili.
- Lazima apite mtihani ili kupokea leseni ya kijana.
- Ona ukurasa wa 4 kwa habari zaidi.

LESENI YA KIJANA

- Kuendesha kati ya saa3 usiku na saa11 asubuhi imewekewa vizuizi.
- Anaweza kuwa na abiria mmoja chini ya miaka 21.
- Haruhusiwi kutumia vifaa vya elektroniki anapoendesha (inatumika kwa madereva wote).
- Hawezi kuendesha katika NYC.
- Ona ukurasa wa 6 kwa habari zaidi.

Kumbuka: vizuizi vya kibali cha kijana na leseni vinatumika eneo ambapo unaendesha, si eneo ambapo unaishi.





Kwa maswali kuhusu chapisho hili au kuagiza nakala, wasiliana na:

New York State Department of Health
(Idara ya Afya ya Jimbo la New York)
Bureau of Occupational Health and Injury Prevention
(Ofisi ya Afya Kazini na Kuzuia Majeraha)
Simu: (518) 402-7900
Barua pepe: injury@health.ny.gov

Kwa habari zaidi kuhusu Sheria ya Leseni ya Dereva ya Kuhitimu, tembelea tovuti ya New York State Department of Motor Vehicles
(Idara ya Magari ya Jimbo la New York):

www.dmv.ny.gov/youngerdriver

Inayofadhiliwa na National Highway Traffic Safety Administration (Idara ya Kitaifa ya Usalama Barabarani) na ruzuku kutoka NYS Governor's Traffic Safety Committee (Halmashauri ya Usalama wa Barabarani ya Gavana wa NYS).

NEW YORK STATE | Department of Health

8239 (Swahili) 5/19